



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**MWALIKO WA WATAZAMAJI WA UCHAGUZI MDOGO WA UDIWANI
KATIKA KATA 32 UTAKAOFANYIKA TAREHE 15 JUNI, 2019**

Kwa mujibu wa kifungu cha 48 (2) cha Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kuendesha Uchaguzi Mdogo wa Udiwani katika Kata thelathini na mbili (32) kwenye Halmashauri ishirini (20) za Tanzania Bara, kujaza nafasi wazi.

Kwa ajili ya kuweka uwazi katika Uchaguzi huo, Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kuzingatia Kanuni ya 14 (2) ya Kanuni za Uchaguzi wa Madiwani 2015, inapenda kualika Asasi za Kiraia na Taasisi mbalimbali za ndani zinazotaka kuwa Watazamaji wa Uchaguzi katika Uchaguzi Mdogo unaotarajiwa kufanyika tarehe 15 Juni, 2019.

Kata zitakazofanya Uchaguzi Mdogo ni: Likuyuseka-Halmashauri (W) Namtumbo-Ruvuma, Kinyasi-Halmashauri (W) Kondoa, Kikombo-Halmashauri ya Jiji Dodoma-Dodoma, Mtowamba, Makuyuni, Majengo-Halmashauri (W) Monduli na Gamako, Daa, Mbulumbulu, Oldeani, Kanssay-Halmashauri (W) Karatu-Arusha, Itenka-Halmashauri (W) Nsimbo-Katavi, Ipole, Pangale-Halmashauri (W) Sikonge, na Itumba-Halmashauri (W) Igunga- Tabora, Boma-Halmashauri (Mji) Mafinga- Iringa, Tandika, Chikongola-Manispaa ya Mtwara Mikindani-Mtwara, Bonyokwa-Halmashauri (W) Ilala, Tungi-Manispaa ya Kigamboni, Chang'ombe-Manispaa ya Temeke- Dar es Salaam, Kitangiri-Halmashauri (W) Ilemela-Mwanza, Ruangwa-Halmashauri (W) Ruangwa-Lindi, Mkula, Lamadi-Halmashauri (W) Busega - Simiyu, Kibosho Magharibi, Uru Shimbwe-Halmashauri (W) Moshi-Kilimanjaro, Murangi-Halmashauri (W) Musoma-Mara, Siuyu-Halmashauri (W) Ikungi-Singida na Kyaitoke, Mugajale, Ruhunga-Halmashauri (W) Bukoba- Kagera.

Asasi/Taasisi zinapaswa kuzingatia masharti yafuatayo wakati wa kuwasilisha maombi yao:-

- (i) Anuani Kamili ya Asasi husika,
- (ii) Anuani ya Makazi ya Ofisi ya Taasisi husika ilipo ,
- (iii) Shughuli ambazo zinafanywa na Taasisi husika kwa mujibu wa Hati ya Usajili ,
- (iv) Kutaja sehemu ambazo Asasi/Taasisi inataka kufanya zoezi hilo la Utazamaji.
- (v) Kutaja idadi ya watu ambao Taasisi/ Asasi itawatumia katika zoezi hilo pamoja na taarifa zao.
- (vi) Kutaja majina na namba za simu za viongozi wa Taasisi husika kama yalivyoandikwa katika Hati za Usajili wa Taasisi.
- (vii) Ikiwa Taasisi inahusisha watendaji wa Kimataifa, wawili lazima wawe Watanzania.
- (viii) Kuambatisha nakala/kivuli cha hati ya Usajili wa Taasisi husika.
- (ix) Kuambatisha nakala/kivuli cha Katiba ya Taasisi/ Asasi husika.

Aidha, Taasisi zitakazopewa vibali vya kuwa Watazamaji zitapaswa kuzingatia Mwongozo kwa Watazamaji wa Ndani ulioandaliwa na Tume kwa mujibu wa Kanuni ya 20 ya Kanuni za Uchaguzi wa Madiwani za mwaka 2015.

Maombi ya kuwa Watazamaji wa Uchaguzi yatapaswa kuwasilishwa Makao Makuu ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi si zaidi ya tarehe 31 Mei, 2019 kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi wa Uchaguzi,
Tume ya Taifa ya Uchaguzi,
Posta House, Ghorofa ya 7,
Mtaa wa Ghana/Ohio,
S. L. P. 10923,

DAR ES SALAAM

Ratiba ya Uchaguzi huo ni Kama ifuatavyo:-

Nä	Tukio	Tarehe
2.	Kutoa fomu za uteuzi kwa Wagombea Udiwani.	27-31 Mei, 2019
3.	Uteuzi wa Wagombea Udiwani.	31 Mei, 2019
4.	Kampani za Uchaguzi Mdogo wa Udiwani.	1-14 Juni, 2019
5.	Siku ya Uchaguzi Mdogo wa Udiwani.	15 Juni, 2019

IMETOLEWA NA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI